

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

Telegrams: "SIASA"
Telephone: 026 2322500
Fax: 026 2323525
(Unapojibu tafadhali taja)



Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Viwanja vya Nanenane Nzuguni
Jengo la Wizara ya Kazi - Mtaa wa Nzuguni A
S.L.P. 2851
DODOMA.

7 Septemba, 2021

TAARIFA KWA UMMA

Nachukua fursa hii kutoa ufanuzi mdogo wa mukutano wangu na waandishi wa habari uliofanyika jana tarehe 06 Septemba, 2021 kwenye ofisi ndogo za Bunge Jijini Dar-es-salaam. Kwenye mukutano huo na waandishi wa habari, nilieleza kinagaubaga/bayana azma yangu ya kuitisha kikao maalum cha wadau wa tasnia ya siasa kutafuta suluhu ya sintofahamu/mivutano iliyojitokeza baina ya Jeshi la Polisi na Vyama vya Siasa hususani vyama vinapotaka kufanya makongamano, mikutano ya ndani n.k.

Kwa masikitiko nimebaini baadhi ya wadau kwa sababu wanazozijua wao aidha kwa makusudi au kwa kutokuelewa vizuri wamepotosha taarifa hiyo kwa kudai kuwa nimetoa amri ya kusitisha mikutano ya ndani ya vyama vya siasa. Hilo halina ukweli wowote na niwasihii mlipuuze kwa uzito unaostahili.

Kimsingi, sijatoa amri ya kuzuia bali nimevishauri vyama vya siasa katika kipindi ambacho tunajaribu kupata ufumbuzi wa mivutano hiyo, ni busara tu ya kawaida kwamba, wakati jitihada zikiendelea vyama vijizue kwa muda kuendelea na shughuli zilizosababisha kutokea kwa mivutano hiyo.

Nitoe wito kwa wadau wote wa tasnia ya siasa nchini kuendelea kuwa wastahamilivu wakati jitihada ikiendelea kuwezesha kikao hicho muhimu kufanyika mapema sana iwezekanavyo ili kupata ufumbuzi utakaokuwa wa kudumu na tija kwa pande zote.

Mungu Ibariki Tanzania.


Jaji Francis S.K. Mutungi
MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA